OFISI YA RAIS TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

SHULE YA SEKONDARI WANGING'OMBE

S.L.P 664, MAKAMBAKO.

TAREHE ……

KUMB.NA.WANGSS/KDTV/ADMN/2021/2022

JINA LA MWANAFUNZI……

S.L.P ……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WANGING'OMBE ILIYOPO WILAYA YA WANGING'OMBE MKOA WA NJOMBE 2021/2022.

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (**Form V)** katika Tahasusi ya ……. Katika shule ya sekondari Wanging'ombe. Shule hii ipo Wilaya ya Wanging'ombe katika kijiji cha Wanging'ombe kando kando mwa Barabara kuu iendayo Mbeya(TANZAM HIGH WAY) ukitokea mji wa Makambako umbali wa kilometa 20. Kwa anayetokea Mbeya, Songwe, Dar es Salaam, Dodoma,Songea na kwingineko mahali pa kushukia ni Wanging'ombe Sekondari utaona kibao cha shule.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe iliyotajwa na serikali na mwisho wa kuripoti ni siku kumi na nne tangu siku ya kufungua shule na si vinginevyo.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2.1 SARE ZA SHULE.

A. WAVULANA.

- Mashati meupe mawili(2) ya mikono mirefu.
- Suruali mbili RANGI YA BLUE BAHARI zenye mifuko miwili pembeni na mfuko mmoja nyuma YENYE TURN UP CHINI.(TAZAMA PICHA –KIAMBATANISHO) NA ISIWE MODAL.
- Sweta mbili rangi dark blue(TAZAMA PICHA)
- Soksi nyeusi jozi mbili
- Nguo za kazi suruali mbili rangi ya Khaki (TAZAMA PICHA) ISIWE MODAL
- T-shirt 2 dark blue yenye kola.(TAZAMA PICHA) na isiwe na maandishi yoyote.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufunika miguu vya kamba visiwe na kisigino kirefu
- Vifaa vya michezo: Track suit blue bahari yenye mkanda mweupe,raba za michezo na jazzy nyeupe ya Real Madrid yenye mikono mifupi.(TAZAMA PICHA).

B. WASICHANA.

- Sketi mbili Blue Bahari **LAZIMA ZIFIKE CHINI YA MAGOTI kama ilivyo katika picha** sketi iwe ya linda box. Tazama picha iliyoambatanishwa.
- Mashati (2) meupe mikono mirefu. (Tazama picha iliyoambatanishwa)
- Sweta 1 rangi ni dark blue(Tazama picha iliyoambatanishwa)
- Soksi nyeupe jozi 2.
- Nguo za kazi sketi 2 rangi ya Khaki (Tazama picha iliyoambatanishwa).
- T-shirt 2 rangi dark blue yenye kola.(Tazama picha iliyoambatanishwa).
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi na kufunika miguu vya kamba.
- Vifaa vya michezo track suit moja blue bahari mkanda mweupe na raba za michezo na jazzy nyeupe ya Real Madrid.(Tazama picha iliyoambatanishwa).

NB: KWA MWANAFUNZI WA KIKE WA KIISLAM ANARUHUSIWA KUVAA HIJABU NYEUPE.

2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE.

a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh. **70,000/=** unatakiwa kulipa Tsh. **35,000/=** kwa muhula au waweza kulipa yote kwa pamoja.

b) Michango inayo paswa kulipwa na kila mwanafunzi.

i) Tsh. 30,000/= ukarabati wa samani-italipwa <u>mara moja tu mwaka wa kwanza.</u>
ii) Tsh. 6,000/= kitambulisho-italipwa maramoja **<u>mwaka wa kwanza.</u>**
iii) Tsh. 20,000/= Taaluma.
iv) Tsh. 10,000/= Tahadhari – italipwa mara moja **<u>mwaka wa kwanza.</u>**
v) Tsh. 30,000/= Kwaajili ya wapishi,walinzi na vibarua wengine.
vi) Tsh.10,000/= Umeme.
vii) Tsh.10, 000/= Huduma ya kwanza.

Tanbihi: Jumla ya ada na michango ni Tsh. 186,000/= kwa mwaka. Fedha hizo zilipwe katika akaunti ya shule benki ya **NMB 60601100017 Wanging'ombe Secondary School**. Hakikisha umeandika jina kamili la mwanafunzi kwenye **Pay In Slip**.

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni

i) Ream ya karatasi 1 (A4) kwa mwaka.
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
iii) Mashuka rangi ya bluu bahari 2, blanketi, mto na foronya rangi ya bluu bahari.
iv) Godoro aina ya Dodoma (2 ½ x 6).
v) Chandarua 2 ½ x 6.
vi) Sanduku la bati au mbao (Tranker) moja lakuhifadhia.
vii) Vyombo vya chakula, Chombo kikubwa cha kuhifadhia maji safi ya kunywa walau cha ujazo wa lita 5.
viii) Ndoo mbili (lita 10).
ix) Leki yenye mpini kwaajili ya usafi wanafunzi wote.
x) Ufagio mmoja softboom wenye mpini(wavulana) na msichana alete mopper (drier) yenye mpini.
xi) Madaftali makubwa yakutosha (Counter books 4 quire).

2.3. **MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA.**

a) Mwanafunzi aje na copy ya cheti cha kuzaliwa.
b) mwanafunzi aje na nakala ya result slip ya matokeo ya kidato cha nne.
c) Kila mwanafunzi atajigharimia matibabu wakati wote awapo nje ya shule.
d) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu ya mkononi shuleni kabisa kwa mawasiliano namba za simu zifuatazo:- **0762055083/0625157446/0752161975.**

OPTATUS MNG'ONG'O
MKUU WA SHULE

3.0 SHERIA ZA SHULE

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana na Elimu nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara tu anapowasili shuleni:-

a) Heshima kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi,wanafunzi wenzie na jamii kwa ujumla
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli(shughuli za kitaaluma na kazi za nje)
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni(evening preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
h) Lugha chafu,matusi,ugomvi,fitina,kupiga/kupigana ni mwiko kabisa kwa mwanafunzi.
i) Wizi wa aina yeyote ni mwiko kwa mwanafunzi.
j) Unywaji wa vileo,kuuza pombe na uvutaji wa aina yeyote ni mwiko kwa mwanafunzi
k) Kuvaa sare za shule wakati wote unapokuwa shuleni((nguo zingine nje ya sare/maagizo ya shule haziruhusiwi)
l) Uharibifu na upotevu wa mali binafsi na mali za umma ni kosa na utawajibika kulipa mali husika
m) Mwanafunzi haruhusiwi kuoa au kuolewa akiwa bado mwanafunzi. Akibainika atafukuzwa shule mara moja. Aidha ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na uhusiano wa kimapenzi. Akibainika atafukuzwa shule.
n) Wageni wataruhusiwa kuwaona /kuonana na wanafunzi baada ya kujitambulisha na kupokelewa na mwalimu wa zamu kila jumapili ya mwisho wa mwezi tu.
o) Ni mwiko kwa mwanafunzi yeyote kwenda nyumba za walimu na wafanyakazi bila ruhusa ya pekee kutoka kwa mwalimu mlezi.
p) **Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na au kifaa chochote kinachohusiana na simu ya mkononi.**
q) Mgomo wa aina yeyote ni marufuku na ni haramu.
r) Mwanafunzi atapokea maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
s) Mwanafunzi atajisafirisha mwenyewe wakati wa likizo au pale atakaporudishwa nyumbani/kufukuzwa shule.

3.2 **MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE.**

i. Wizi.
ii. Uasherati,ushoga,ubakaji,kuoa au kuolewa
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama cocaine,kubeli nk.
iv. Uvutaji wa sigara.
v. Kupiga au kupigana kwa mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote na makosa mengine ya jinai.
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
vii. Kudharau bendera ya Taifa.
viii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako,walimu au walezi na jamii kwa ujumla
ix. Kugoma kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
x. Kukataa kwa makusudi adhabu.
xi. Kumiliki simu ya mkononi shuleni.
xii. Kushiriki au kuendeleza imani za kishirikiana
xiii. Kunyanyapaa au uonevu wa aina yeyote
xiv. Kuweka mimba au kupata mimba
xv. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 60 bila taarifa/utoro

xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xvii. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kama kunywa sumu n.k.

FOMU NA.1 KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI.

A: MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI……
2. Shule ya "O"level uliyosoma……..
3. Namba ya mtihani ……
4. Tarehe ya kuzaliwa…….
5. Nakubali nafasi niliyopewa/sitaki apewe mwingine (kata lisilohusika)
6. Nakiri/naahidi kutoshiriki migomo,fujo na makosa ya jinai
7. Sahihi ……..

B: AFISA MTENDAJI

JINA……

KIJIJI/KATA……..Wilaya …….Mkoa……

Nathibitisha kuwa mwanafunzi ……ni mkazi wa kijiji/mtaa/kata hii na ni raia wa Tanzania.

Sahihi ……Muhuri ……tarehe ……

C: MZAZI/MLEZI

JINA……

Nakubali mwanafunzi apate Elimu yake hapo Wanging'ombe sekondari na kwamba atafuata sheria,kulipa ada,michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule na vinginevyo aadhibiwe. Pia atalelewa katika dini ya …….

FOMU NA.2. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI.

JINA LA MWANAFUNZI……
TAREHE YA KUZALIWA……
JINSIA……UMRI……
MAHALI
UNAPOISHI……WILAYA……MKOA……
SIMU NA……
JINA LA BABA……..……..YUPO HAI?.....
JINA LA MAMA……YUPO HAI?.....
ANUANI ……
SIMU NA…….
KAZI YA MZAZI/MLEZI ……

NB: TAARIFA ZA UONGO/ZISIZO SAHIHI ZITAPELEKEA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

FOMU NA.3. MEDICAL EXAMINATIONS.

(To be completed by medical officer only)

1. Pupil's name …….
2. Age……..
3. Blood count (white and red)…….
4. Stool examination ……..
5. Syphilis or/and other venereal diseases test ……
6. T.B test ……..
7. Eye test ……..
8. Ears ……..
9. Abdomen ……
10. Spleen ……..
11. Urine for plamo test …….

ADDITIONAL INFORMATION

If any e.g physical defeats,impairment,infections,pregnancy,chronic or family diseases etc

……

I CERTIFY THAT THE ABOVE IS FIT TO PURSUE FURTHER STUDIES IN EDUCATION

STATION……SIGNATURE…….

DATE……..DESIGNATION……OFFICIAL STAMP……..

FOMU NA.4. PLEASE IF POSSIBLE COME WITH THE FOLLOWING BOOKS/REFERENCE/MATERIALS RELEVANT TO YOUR COMBINATION AS LISTED BELOW.

1. **HISTORY**
   i. Essentials in Advanced Level History Paper 1&2 ……. By Saleh Yassin
   ii. Major events in African History ……..by Mwijage
   iii. Africa since 1800- 4th edition
   iv. The marking of modern Africa
   v. How Europe under develop Africa
   vi. Europe from 1815 ……by Peacock
2. **Geography**
   i. Certificate of Geography (oxford) …….by mary Mugo.Robert Kamugat and Paul kibuuka
   ii. General Geography in diagrams …… by R.B bunnet
   iii. Photography interpretation and elementary surveying for secondary A level
   iv. Certificate human and economic Geography ……..by Morgan and Leong Ghang
3. **English Language**
   i) Advanced Englisha Language I by Ndambo C.S & Kinunda
   ii) English language I by Asheri N.
   Plays
   i) Betrayal in the city – Francis Imbuga
   ii) I will mary when I want -Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii
   iii) An enemy of the people- Henrick Ibsen
   Novels & short stories
   i) Encounters from Africa – macmillan education Ltd
   ii) Beautiful ones are not yet born – Anyi kwei armah
   iii) His excellency the head of state- Danny safo.
   Poetry
   i) Selected poems – Institute of education
   ii) The wonderful surgeon and other poems- Charles Mloka.
4. **General Studies**
   i) Understanding advanced level general studies by J.Bigirwamungu $ S.Deogratius
   ii) General Studies Notes (for A-level form V-Vi)……..By Mshiu and Nyangwine
5. **Kiswahili**

Ushairi

i. Kimbunga ……..G.Gorn (TUKI) 1994
ii. Changu Tamu …….T.A Mvungi
iii. Mapenzi Bora …… S. Robert

Riwaya

i. Vuta N'kuvute ……Shafi A Shafi
ii. Kufikirika ……S.Robert
iii. Mfadhili ……..Hussein Tuwa
iv. Usiku utakapokwisha……Mbunda Msokile

Tamthilia

i. Morani ……. E Mbogo
ii. Kivuli kinaishi …….. Said Mohamed
iii. Kwenye ukingo wa Thim ……. E Hussein
iv. Nguzo mama …… (DUP) 1982.

A. **SARE YA WASICHANA.**

PICHA 1. SARE YA DARASANI PICHA 2. SARE YA KUSHINDIA NJE YA DARASANI. PICHA 3. SARE YA MICHEZO. PICHA 4. SARE AKIWA AMEVAA SWETA. PICHA 5. TRACK SUIT

1 **2** **3** **4** **5**

B. **SARE YA WAVULANA**

PICHA 1- SARE YA DARASANI SHATI JEUPE MIKONO MIREFU

PICHA 2. SARE YA KUSHINDIA NJE YA DARASANI PICHA 3- SARE YA MICHEZO PICHA 4. SARE AKIWA AMEVAA SWETA PICHA 5. TRACK SUIT

1 **2** **3** **4** **5**

ANGALIZO KUU.

1. NI MARUFUKU SURUALI KUWA YAKUBANA CHINI. (MODAL STYLE)

2. SKETI NI LAZIMA IWE NDEFU SANA KAMA MCHORO ULIVYO AU ZAIDI.